




MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

Na. 20. Msimu wa kilimo 2019/2020 Tathmini Aprili 11-20, 2020 na matazamio kwa kipindi cha Aprili 21-30, 2020


Muhtasari

- Mazao yanaendelea vizuri kutokana na mvua zinazoendelea.
- Wakulima wanashauriwa watumie dawa kwenye mazao yaliyoathirika kutokana na fangasi waliosababishwa na unyevunyevu wa udongo uliokithiri
- Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kufuata ushauri wa maafisa ugani kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2020

Katika dikadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) ilipungua nguvu wakati ile iliyopo kusini (St. Helena na Mascarene) iliimarika. Hali hiyo imesababisha kusukumwa kwa ukanda wa mvua kuelekea kaskazini mwa nchi. Uwepo wa Joto la bahari la juu ya wastani katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Madagascar) lilisababisha kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa. Katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) kulikuwa na joto la bahari la chini ya wastani, hali iliyopelekea kuwa na mchango mkubwa katika kuleta upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea kwenye baadhi ya maeneo ya nchi. Uwepo wa migandamizo midogo ya hewa na joto la chini ya wastani kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki kulikua na mchango mkubwa wa mvua kwa baadhi ya maeneo nchini.

MWENENDO WA MVUA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2020



Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Aprili 11-20, 2020

TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2020

Maeneo mengi ya magharibi, ukanda wa ziwa Viktoria na na pwani ya kaskazini yamepata mvua nyingi kuliko maeneo mengine ya nchi (angalia Kielelezo). Kiasi cha mvua cha zaidi ya mm 250 kimererekodiwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani na visiwa vya unguja na Pemba. Hata hivyo upungufu wa mvua umeonekana katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua ampapo kiasi cha chini ya mm 10 kilipimwa katika mikoa ya Ruvuma, Rukwa na Singida kama inavyoonekana katika Kielelezo.

Katika kipindi cha dekadhi iliyopita, mazao yameendelea vizuri kutokana na mvua za msimu zinazoendelea. Maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua kwa mwaka, mahindi yalikuwa katika hatua ya kubeba na kukomaa. Wakulima katika mikoa ya Iringa, Njombe, Mbeya, Dodoma, Singida, Tabora na Kigoma waliendelea na shughuli za uvunaji wa Maharagwe na pia athari za fangasi zimeonekana kwenye maharage katika baadhi ya maeneo mengi kutokana na unyevunyevu uliokithiri kwenye udongo. Kwa maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hususan mikoa ya Mara, Kagera, Morogoro na Arusha mahindi yapo

katika hatua ya jani la tatu na jani la tisa, na pia wakulima waliendelea na shughuli za palizi pamoja na upulizaji wa dawa za kuua wadudu waharibifu kwenye mimea. Vilevile, katika mkoa wa Kagera maharagwe yameharibiwa na mvua nyingi zinazoendelea kunyesha. Aidha, maeneo machache ya ukanda wa pwani wa kaskazini (Morogoro, Tanga, na visiwa vya Pemba, na Unguja) zao la mpunga lilikuwa katika hatua ya kutoa maua. Hali ya unyevunyevu katika udongo na malisho kwa ajili ya wanyama ilikuwa ya kuridhisha.

**HALI YA MAJI ILIVYOKUWA KATIKA
KIPINDI CHA APRILI 11-20, 2020**

Kiwango cha maji katika mabwawa na kutiririka kwa maji katika mito vimeongezeka katika maeneo mengi ya nchi kutokana na mvua za masika na msimu zinazoendelea.

**MIFUMO YA HALI YA HEWA
INAVYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA
APRILI 21-30, 2020.**

Mifumo ya migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kaskazini mwa dunia itaendelea kupungua nguvu, wakati ile iliyopo kusini itaendelea kuongezeka nguvu. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuuweka ukanda wa mvua kaskazini mwa nchi. Joto la bahari la juu ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la kusini magharibi mwa bahari ya Hindi (kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki, karibu na pwani ya Angola). Hali hii inatarajiwa kusababisha vipindi vya migandamizo midogo ya hewa kusini magharibi mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuimarisha upepo kuvuma kutoka magharibi (katika misitu ya Congo) kuelekea maeneo ya nchi yetu, hivyo kuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha mifumo ya mvua katika baadhi ya maeneo ya magharibi, ukanda wa ziwa Viktoria, pwani ya kaskazini pamoja na kaskazini mwa nchi.

**HALI YA HEWA INAVYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2020.**

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mkoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na pwani ya kaskazini (mkoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua katika baadhi ya maeneo.

Nyanda za juu kaskazini mashariki (mkoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro), magharibi mwa nchi (mkoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) na kanda ya kati (mkoa ya Dodoma na Singida) yanatarajiwa kupata mvua katika baadhi ya maeneo hususani nusu ya kwanza ya dekadini.

Nyanda za juu kusini magharibi (mkoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) kunatarajiwa kupata vipindi vya mvua katika maeneo machache.

Pwani ya kusini (mkoa ya Mtwara na Lindi) na kanda ya kusini (Ruvuma na kusini mwa mkoa wa Morogoro) yanatarajiwa kupata vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

**HALI YA HEWA KILIMO INAVYOTARAJIWA
KATIKA KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2020**

Hali ya unyevunyevu katika udongo inatarajiwa kuendelea kuongezeka katika maeneo mengi yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka, hali ambayo itasaidia ukuaji na maendeleo ya mazao. Hata hivyo hali ya unyevunyevu uliokithiri hususan katika baadhi ya maeneo umesababisha Fangasi kuathiri mazao hivyo wakulima wanashauriwa kutumia dawa za kuzuia magonjwa kwenye mimea. Hali ya unyevunyevu katika udongo na malisho kwa wanyama vinatarajiwa kuwa vya kutosha katika maeneo mengi ya nchi. Wakulima, wavuvi na wafugaji wanashauriwa kuwasiliana na maofisa ugani kwa matumizi sahihi ya utabiri huu.

**HALI YA MAJI INAVYOTARAJIWA KATIKA
KIPINDI CHA APRILI 21-30, 2020**

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kuongezeka katika maeneo mengi ya nchi. Hata hivyo, watumiaji wa maji wanashauriwa kuendelea kuyatumia kwa uangalifu na kuchukua tahadhari juu ya majanga yaletwayo na mafuriko.

Jarida limetayarishwa na:

Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania

Ghorofa ya 3-Ubungo Plaza – 388 Barabara ya Morogoro,

S.L.P 3056; 16102 Dar es Salaam, Simu. 255 -(0) 22 – 2460706-8; Nukushi: 255 - (0) 22 – 2460718 ; Barua pepe: (1) met@meteo.go.tz (2) agromet@meteo.go.tz; Tovuti:

www.meteo.go.tz, -Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania